

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

Verbatim Report Of

DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL,

NTONYIRI CONSTITUENCY, HELD AT LARE MULTI PURPOSE HALL

ON

OCTOBER 11, 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, NTONYIRI CONSTITUENCY HELD AT LARE MULTI
PURPOSE HALL 2002.**

Present:

1. Com. Domiziano Ratanya - Chairman

Secretarial Staff Present:

1. Solomon Anampiu - Program Officer
2. George Kimanthi - District Coordinator
3. Assist. District Coordinator
4. Mary Babu - Verbatim Recorder
5. Members of 3Cs

The meeting was called to order at 10:00 a.m with Com. Domiziano Ratanya in the Chair.

George Kimanthi - District Coordinator: Nafikiri tutaanza, naona watu wanakuja halafu wanaenda, tuanze na wale wako, na wale watatupata tukiendelea mtawaelezea ama watasoma baadaye si ni hivo? Kwanza kabisa tutasema ya kwamba, mara ya mwisho tulipokuwa hapa ilikua mwezi wa tano, tarehe kumi na tano mwezi wa tano. Ndio tulikuwa hapa tukachukua maoni yenu, na kama mulivio ambiwa ni kwamba hayo maoni yenu, yametayarishwa, yamerudishwa katika drafts. Kuna wanaiita kichoro, Draft Constitution ama kielelezo cha Katiba, na hiyo Draft ilioko ni kwamba leo tuko hapa kwa ajili ya kujadili na

kisha nyinyi wenyewe, muache tuwasomee

(inaudible) kwa makanisa (interrupted by noise). Kwa hivyo leo

tuko na Commissioner na wengine kutoka headquarter ambao wanatengeneza hii Katiba, lakini kabla hatujaendelea ningeomba mmoja wenu atuongoze kwa maombi. A volunteer? Tuko na pastor.

Rev. Akule N’lthai - (prayer): Natuombe. Ewe Mwenyezi Mungu, mwenye rehema na

neema, twainua jina lako takatifu, kwa kuwa wewe ndiye mtakatifu pekee. Na kwa hivyo Baba, sisi tuko mbele yako watoto wako wanyenyekevu, tukiomba utusamehe dhambi zetu, ili nasi Baba ukatusafishe, na ukatuweka safi mbele ya macho yako kwa sababu unapenda kutumikiwa na watoto walio watakatifu. Kwa hivyo twakuita ili Baba uwe pamoja nasi, ukatuweka tayari kimawazo, ukatuweke tayari kimwili na kiroho, ili katika kazi ile iko mbele yetu ya Katiba yetu, Baba tutaichangilia, tukapeane maoni tukiwa tunaongozwa na Roho Mtakatifu, tukijua kazi ile tunafanya Mwenyezi Mungu ni ya kufanya nchi yetu, iishi vizuri, na hata mambo ya kuitawala iweze kutawaliwa kwa haki na kwa njia iliyo nzuri, na katika kukata national cake, Baba iende ikafanywe kwa haki, na kwa kila mmoja akatendewe haki yake.

Kwa hivyo Baba, twakuomba uwe pamoja nasi, ukatusaidie kwa kazi lolote lile tutakalo tenda hapa siku hii ya leo, ili Baba tukitoka hapa tuwe tumefanya yale yatafanya serikali yetu, ifanye kazi ile uli-iita ikawepo, ili nchi ya Kenya ikae kwa amani, iweze kufanya maendeleo yale yatafaidisha kila Mkenya, na kila Mkenya aone faida na hata akujue kwa sababu nchi hii ni yako, na vyoyote vilivyo ndani ya nchi hii ni vyako.

Kwa hivyo Baba kabla ya kufanya chochote twaomba ruhusa ukatuongoze nasi tukatenda kazi ile italeta sifa katika jina lako, na hata serikali yetu ikawa na viongozi, wale watakuwa wakielekezwa katika kazi zao, wakiongozwa na Roho Mtakatifu wako kwa kufwatilia Katiba iliyo ya haki, na iliyo na sheria zile zitaleta amani miongoni mwetu sisi zote. Utubariki kwa kuwa sisi ni watoto wako. Twaomba haya tukiamini hata yale mengine ambayo hatujayataja, unayajua na utatimiza yote kwa mapenzi yako, na katika jina la Bwana Yesu Kristo tumeomba Amina.

Audience: Amen.

George Kimanthi-District Coordinator: Asante sana. Kabla sija mualika Com. Domiziano Ratanya, ningetaka kutambulisha wana kamati wa 3Cs, ambao wako hapo. Tuko na Chairman Julius Gaithuru.

Julius Gaithuru- 3Cs Chairman: Inaudible

George Kimanthi: Tuko na Doris Mwendwa.

Doris Mwendwa: Inaudible.

George Kimanthi: Tuko na Nathan Kunja, na kuna Councillor pale ambaye ni a Amos Kiumo. Amos ni Delegate, yule ataenda National Constitutional Conference kutoka Nyambene. Kwa hivyo yuko pale. Then tuko na Beatrice Bario yeye ni delegate mwingine kwa upande wa akina mama ambaye ataenda kule National Constitutional Conference na amejiunga nasi leo. Amesema ni lazima ajiandikishe nanyi na aangalie huko.

Kwa hivyo sina mengi lakini nawaambia msikize kwa makini yale mtaelezwa na kama kuna swali, kama kuna mahali hamuelewi, Commissioner ako hapo, yuko na Program Officer, ndiye atawaelezea kwa uzuri, lakini hata nyinyi muwe mnaelewa zaidi, na muweze kufundisha wengine.

I want to go to Commissioner Domiziano Ratanya.

Com. Domiziano Ratanya: Okey. Asante sana Bwana Coordinator, wananchi wa hapa Ntonyiri Constituency, hamjambo wote? Siku ya leo, katika mkutano wetu, pengine nafikiria tukubaliane tutumie lugha ya Kingereza ama Kiswahili na ukiwa huwezi kabisa, unaweza kuongea lugha yako ya Kimama, na halafu tutakuwa tunatafsiri. Na ikiwezekana, nauliza ni heri mtumie Kiswahili badala ya Kimeru, kwa sababu tuna yule officer ambaye anafanya recording hapa ambaye nitawajulisha baadaye, hawezi kuelewa Kimeru kwa hivyo mnajua lugha ya Kiswahili ndiyo national language. Kwa hivyo ukitumia Kiswahili, ni vibaya kutumia Kiswahili? Mnakubali tutumie Kiswahili? Mkitumia Kingereza sana kuna wengine ambao hawataelewe, lakini una uhuru wa kuongea Kingereza na Kiswahili.

Kwanza ningetaka kuwajulisha ile team ambayo nimekuja nayo kutoka huko Secretariat yetu kutoka headquarters ya Constitution of Kenya Review Commission. Mmoja upande wa kushoto hapa, ni Solomon Anampiu ambaye ni Programme Officer wetu.

Solomon Anampiu: (inaudible)

Com. Domiziano Ratanya: Okey asante sana Bwana Anampiu. Mwingine ambaye tunaye ni Mary Babu ambaye anafanya recording na kuandika. Na hata ana tape recorder ambayo anatumia huwa ananasa mambo yote ya recording, yaani maneno yale mnazungumza. Na mimi naitwa Domiziano Ratanya, Commissioner, na ni mmoja wa wale ambao walikuja hapa kuchukua maoni yenu, nilikuwa hapa, sikuwa na Commissioner mwingine, na mimi nimetoka hapa upande wa Nyambene tunapakana na Imenti, upande wa Tigania ----, hapo ndiyo kwangu nyumbani. Kwa hivyo mimi ni mtu wa Meru North.

Na kwanza ningetaka, kabla ya kuendelea na mazungumzo zaidi, kuwajulisha ni kwa nini tumekuja hapa. Mnajua Commission imekuwa ikija kwenu wakati mbali mbali, na tena iliwapatia officers ambao mnatumia, ambao wanawatumikia nyinyi na mnafanya kazi pamoja. Wakati nilipokuwa hapa tulikuwa tunachukua maoni yenu, ili tuweze kuyatumia kwa kufanya

Constitution ya Kenya Review, ama kubadilisha yale wananchi wanataka yabadilishwe katika Katiba. Mkatupatia maoni yenu na tulienda Constituencies zote katika Kenya. Zote ni 210, mia mbili na kumi, pahali wabunge wanawakilisha.

Na tulipoenda kwa zote kabisa tulichukua maoni, tukaenda tukayaweka pamoja, tukayaangalia vizuri kwa wakati mrefu tukiwa Commissioners, na baadaye tukakubaliana yale tutaingiza kwa Katiba mpya kutokana na maoni yenu.

Ukiangalia hapa kwa hii file, utaona hapa kuna Constituency No. 48 ni Ntonyiri Constituency. Yale maoni mliyo tupatia yako hapa. Maoni yenu ambayo mlikuwa mnataka yawekwe Katiba. Tulifanya summary yake iko hapa na kwa kila Constituency ingine tulichukua maoni tukaweka pamoja na halafu tukafanya mapendekezo ya Constituency hii. Mapendekezo ya Constituency ama Katiba mpya, tuliyafanya kwa njia mbili. Pendekezo la kwanza, hii ilikuwa report ya vile kazi ilikuwa inaendelea. Na kwa hii Kitabu tunaita People's Choice ambayo ilitangazwa kwa magazeti baada ya tarehe 18 mwezi wa tisa na halafu baadaye tukaweka kwa kitabu. Hizi vitabu hazikuwa nyingi sana lakini pengine baadaye mtapata vitabu. *To Secretariat staff (Do you have any copies?)*

Secretariat staff: (inaudible)

Com. Domiziano Ratanya: Very few?

Secretariat staff: (inaudible)

Com. Domiziano Ratanya: Documentation Centre? Okey do you have for them here or there?

Secretariat staff: At the office.

Com. Domiziano Ratanya: Kwa hivyo tuli-produce copies tukaenda kwa Documentation Centres. Na hii ni copy ambayo ni report kuona ile kazi Commission ilikuwa inafanya. Na hii ilitokea tarehe kumi na nane mwezi wa tisa, ilikua Mombasa. Kutokana na hii repoti fupi, tukaanza tukaendelea tukatengeneza Constitution yenyewe ambayo tunaita Draft Constitution. Na hiyo Constitution tukaiandika, tukaitoa tarehe ishirini na saba mwezi wa tisa. So this is when we launched the draft. But I have told you we launched the report on 18th, ilianza wakati huo na hata ikaingia kwa magazeti, watu wakaanza kusoma kwamba Commission imemaliza kazi ya Constitution na sasa wanaendelea kufanya draft yenyewe.

Draft ni ile inaingia ili wakati itakuwa Kitabu na baada ya kuandaliwa na National Conference na Parliament, iwe ndiyo Katiba. Sasa yale mambo ambayo yako hapa ni yale ambayo yatatengeneza Katiba. Hii tu ni report kwa sababu ukienda kusoma hivyo ukiangalia kidogo hii, ukiangalia kwa hii pengine utaona majina ya Commissioners wako hapa na mipango yote, lakini hiyo sio Katiba, majina ya Commissioners siyo Katiba ni wafanyi kazi hawa na kwa hivyo ndiyo report.

Lakini hapa hutaona Commissioners, utaona mapendekezo ya kufanya Constitution yenyewe, utaona mapendekezo mengi.

Tutaangalia kidogo, utaona kuhusu utalawa, kama ni mambo ya mashamba, kama ni mambo ya citizenship, mambo mengine yote utayaona hapa kama vile mlikuwa mnazungumza.

Sasa tulipo peana hii kwa Kenyans tarehe ishirini na saba, na tarehe 30 September, tukapeleka Parliament, Commissioners wakakubaliana wakasema ni heri tuende kwa Constituencies zote pale tulichukua maneno, tuwaambie sasa waendeleo kuzungumza, ku-debate na kuongea mambo kuhusu mapendekezo ya Katiba. Kwa hivyo leo ni launching, tumekuja kuanza, muanze kusoma. Na hii nitasoma thirty days, kwa sababu sheria inasema, draft ikiwa tayari itasomwa siku thelathini kutoka wakati ilikuwa launched kutoka 27th September mpaka siku thirty, that is 27th October. Na tarehe 28th October, tutakuwa sasa na mkutano wa National Conference, mkutano wa Wajumbe wenu ambao wanaenda huko Nairobi, waketi mwezi mmoja wakikagua haya maneno ambayo yameandikwa na Commissioners kutokana na maoni ya wananchi.

Wakiona kuna hitilafu yeyote, hawa delegates, watabadilisha. Wakiona wachukue kama vile ilivyo itaendelea, wakiona wataongeza, wanaweza kuongeza. Mnaskia kwamba mpaka sasa watu wanazungumza haya maneno. Watu wa madini, watu wa business, politicians, wote wanaendelea sasa kuzungumza. Lakini tulisema kwa sababu tulikuja kwa Constituencies, Commissioners waje hapa hapa, wa-waambie sasa tunawapatia hii copy, sasa hata nyinyi endeleeni kusoma. Na mkisoma mkiona maoni yenu mtatuambia baadaye.

Kwa hivyo maana ya siku ya leo ni kuja kuanza kusoma hii draft, muanza na tunakuja hapa kwa Ntongiri Constituency, ili tuwajulishie kwamba iko tayari na nyinyi muendeleo sasa na mazungumzo yenu within the Constituency. Muungane na Wakenya wengine kuzungumza haya mambo yenye yako katika draft mpaka tarehe 27th, 28th ikifika, muwe mmemaliza na mmetoa mapendekezo yenu. Sasa hiyo ndiyo sababu kubwa sana ya kuja hapa. Sisi tukizungumza hapa kidogo tukiwaachia hii, mtaendelea kusoma nyinyi wenyewe na mtatoa maoni yenu. Na ningetaka kuwaambia kabla sijaendelea kuzungumza zaidi, si kusema yenyewe ni Katiba, lakini ni mapendekezo ya kufanya Katiba. Katiba itatokea baadaye kutokana na haya maneno yako hapa. Na ikitokea, ikikubaliwa na ikifanywa sheria iwe Katiba, itaandikwa kwa vitabu kama hili mnaona hapa. Kitabu namna hii ni kitabu ya Katiba ambayo tunatumia sasa.

Sasa hata hii mnaona iko katika karatasi ya newspaper. Commission iliona kwamba kwenda kuandika hii kwa Kitabu kama hiki itakuwa pesa nyingi sana na tena mambo hayajaisha, ni draft tu itakuwa pesa nyingi sana. Ama ukiandika kwa hii Kitabu yenyewe ile muundo wa kitabu ya sheria, itakuwa pesa nyingi na si mwisho. Kwa hivyo hii si mwisho, it is not final. Hata mkiona imeandikwa kwa gazeti si final, lakini kile muhimu ni kwamba iandikwe ile uone maneno hapa mkasome myazungumzie na ikifika wakati wa kuandika final, Commission itaona ule muundo ambao itaandika, kama ni namna hii, ama namna hii, ama namna ingine, ile ambayo itawezekana na ile itakubaliwa baada hata ya kutoka kwa Bunge.

Kwa hivyo msiseme Katiba iko katika newspaper ama karatasi. Mnaona hapa imeandikwa draft. Draft ni kama pendekezo la kwanza ambalo tutakuja kuandika mwisho. Yaani tuandike ile copy yenyewe ambayo ni ya mwisho. Hii ni ya kutusaidia tuanze

kusoma na tena tukaona hata kununua hii itakua rahisi kwa Commission badala ya kutengeneza kitabu kama hiki na hii mambo haijakuwa mwisho.

In Kenya every where pale Commissioners wako, kwa sababu leo kuna wengine wako huko Tharaka, kuna wengine Siakago kuna wengine Kisumu. Sisi sote tumeenda nje, hakuna Commissioners wamebaki huko, tumewagawanya mmoja mmoja ama wawili wawili lakini mainly ni mmoja mmoja, akiwa na Program Officer na Officer mwingine. Sisi sote twenty-nine tuko nje. Twenty seven Commissioners and two ex-officio Commissioners wako wote nje, na makaratasi haya yakienda Kenya yote hata hii lot yenyewe tulinunua na pesa nyingi. Kwa hivyo hii ikimaliza kazi tutakuwa na muundo wa Kitabu. Mkiuliza hiyo swali mtaona sasa kuna sababu.

Na kwa kuanza sasa hata nikiketi kwa sababu tutaulizana hata maswali. Nitaanza kwanza kuangalia hii. Yaani hii repoti yenyewe ingawa hamna hii, kwa sababu nawaambia hii si Draft Constitution lakini ni report kuwakumbusha vile tulianza kazi yetu. Na utaona kwamba sitakuwa nasoma page kwa page, hakuna wakati huo; lakini nikupeana ile high-light kuonyesha ya kwamba, kila point ilifanyika.

Na tukiangalia kwa hii short report, utaona ya kwanza watu wa Kenya walitaka Katiba ibadilishwe. Ukiendelea kusoma hapo utaona, na wakaamua wawe na Commission yenyewe. Kwanza kulikuwa na Commission ya Commissioners kumi na watano mwaka wa 2000. Halafu baadaye mwaka wa 2001, Commissions zilikuwa mbili, zikaungana 2001, zilipoungana kutoka June, 2001 ikandelea sasa ikiwa Commission moja ya wajumbe twenty-seven, na mimi nikiwa mmoja wao na ex-officio Commissioners wawili, mmoja ni Secretary P.L.O Lumumba na mwingine ni Attorney General. Sasa hayo yako hapa kwa hii report.

Na nikiendelea kwa background ingine ni kwamba, tuliendelea tukasema tufundishe watu, ikiwa stage ambayo tunaita Civic Education and that was preparing the people for participation. Commission ikaketi ikasema tuwe na Civic Education. Civic Education ni kufundisha watu wajue ni kitu gani kinaendelea. Kwa Civic Education, tulikuwa na taabu nyingi hapo kukubaliana, kuna stage makanisa walikuwa wanasema wanataka kufanya Civic Education kila pahali, kuna watu hata kutoka mbali kama Ulaya walikuwa wanasema wao ndiyo watafanya Civic Education, waingie kwa nyinyi huku waifanye.

Kulikuwa na maneno mengi ambayo watu hawakukubaliana, tukaona kitu kizuri ni Commission yenyewe iangalie ifanye Civic Education. Kwa sababu kama watu wangezunguka huko NGO's kama ni Wazungu kuja huku ingekuwa maneno mengi sana, sindiyo? Wazungu wangeanza mambo mengi, pesa pengine ingejaa huku, ingekuwa inamwagwa huku, lakini pengine tungepitia kweli Katiba kwa njia hiyo, na tumejitawala? Sasa tukaona kukubaliana na hawa ma-NGO's makubwa makubwa, watu wengi waingie hivi, haingekuwa vizuri, mpaka Commission yenyewe ikasema iulize watu wa-apply wale wanajua wanaweza kusaidia kufundisha wananchi, na wawe katika group and in that way involving everybody. Sasa wanaandika barua wengine wakiwa Youth Groups, wengine makanisa, wengine hata Njuri Njeke wali-apply na walimu retired na hata retired officers, wengi wengi wali-apply.

Kama Nairobi kulikuwa na providers kama, I think about (how many Bwana nani, Nairobi yenyewe?)

Answer: (inaudible)

Com. Domiziano Ratanya: Yes mnasikia, kama Nairobi ilikuwa karibu 2,070, one Constituency. Ha hiyo haikuwa mtu mmoja, ni groups. Na unajua group inaweza kuwa na watu kumi, ishirini na hata forty, hii ilikuwa Nairobi katika Constituency moja, na najua Nairobi ina nyingi kama nane hivi. Constituency kama hii, sijui kama walikuwa providers kama kumi ama kumi na---- (walikuwa wangapi hapa anake?) about nine? Si unaona ni tofauti tofauti. Sasa hapo walipoanza kufundisha na ningetaka kutaja hapa juu ya pesa ya Civic Education, pesa yenyewe ile Commission ilipata haikuwa nyingi ya kutosha ya kulipa hao wote, kwa sababu walikuwa wengi na tulisema wananchi wahusike, otherwise tungenesema yakae tutumiwe mabarua kama haya na mambo yaishe. Ama Commissioner aje siku moja azungumzie hapa halafu tusema Ntonyiri imejua. Si kama sasa mimi nimeongea leo, kuna providers wanaenda round kuwafundisha? Hii mambo itaishia hapa launching. Lakini kama Civic Education tungefanya hivyo, sijui kama ingekuwa vizuri sana kwa sababu mgetaka participation muendeleo hata nyinyi kuzungumza kwa nyinyi wenyewe kwa vijiji.

Tukasema ni heri muwe na hizo groups, lakini pesa ile ilipatikana na mkalipwa ndiyo ilikuwepo, ndiyo Commission ilikuwa nayo.

Na ile Co-ordinator alilipa ilikuwa accounted kule Nairobi na Secretariat, na ikaonekana alitumia kiasi ambacho alipatiwa. Haikutosha, na sio Ntonyiri pekeyake, everywhere haikutosha kwa sababu ile Commission yenyewe ilipata ilikuwa kianzisho na ikagawana kila pahali katika Kenya, lakini tuliwashukuru wengi waliofanya kazi kama voluntary na ikawa kiwango ambacho tulikuja tukakusanya maoni kama haya unaona tumeandika hapa. Kwa hivyo hiyo ilikuwa stage moja na ilifanywa vizuri, isipokuwa kama vile nawambia malalamiko yalikuwako ya pesa na haikuweza kutosha kwa vile ile iliyopatikana ndiyo ililipwa.

Then kwa hii report kuna “What the people told us” tukiangalia hapa utaona watu walitumbia, mambo mbali mbali na kutokana na maoni ya watu, yale ambayo yamewekwa hata kwa Katiba, yale ambayo wananchi walisema ni mengi na ndiyo tumeandika kwa kila Constituency tofauti tofauti. Nikiangalia hapa katika page moja “What does the Draft Constitution do for Women?” for example here tunaona inaandika it prohibits discrimination on grounds of sex, pregnancy, marital status, requires new laws to make this effective. Due account must be taken of needs to include women in public bodies and judiciary and so on. Political parties must be democratic including and getting the involvement of women.

Hii ni mfano tu ya yale machache ambayo yalikuwa yanasemwa, yalisemwa kwa kama kuhusu disability. For example hapa, discrimination on girls of disability is prohibited. This is a common consensus everywhere. It should not discriminate disabled people or people with disability. This ofcourse is a point that covers everywhere and we had a lot said about that one in Ntonyiri Constituency, if you go through what Ntonyiri people said.

Mfano mwingine about human rights, watu walisema mambo mbali mbali ya watu ambao ni maginalised. Walisema mambo ya

women, walisema mambo ya youth. Walisema mambo ya children, walisema mambo ya the aged, ama wazee ambao wame-retire, ama wale hawajafanya kazi ya serikali lakini wako nyumbani wame-retire hawafanyi chochote, ni wazee sana. Hayo yote, na hata right yako wewe mwenyewe, which is not given by the Constitution, but God given right should be protected and if I check an example here on this is page 18 of this book. “How is the New Constitution different from the old?” Wakati mwingine watu wanauliza ni mambo gani yamegeuka kutoka kwa old Constitution, yaani kitabu kama hiki nimewaonyesha. Hii ni Constitution yenyewe kwa sababu ilimaliza mambo yake yote wakati wake na ndiyo tuna-revise, ndiyo tunaendelea kubadilisha badilisha. Na nikisoma machache hapa kwa yale yamebadilika ama ni tofauti kidogo, nikichukua mfano mmoja hapa Parliament consists of two Houses, under the National Assembly and the National Council, that is about the new proposal that will appear in the new Constitution, that the Parliament is going to have two chambers, the Upper House and the Lower House. I will give you the names National Assembly and the other one is National Council. But what about the old Constitution?

There is only one Parliament, just House of representatives, that is National Assembly, lakini tulipo nyakua Uhuru 1963 and around 1964, kulikuwa na two Houses. Kulikuwa na Upper House ambayo ilikuwa inaitwa Senate na kulikuwa na Lower House, ilikuwa inaitwa House of Representatives ama Lower House. Naona sasa hiyo ilikuwa zamani, 1963 lakini kutoka 1964, 1965 kuendelea hapa, kulifanyiwa amendment kwa Constitution ya kwanza, hayo maneno yakaondolewa, nakumbuka kulikuwa na Mjumbe mmoja ambaye anatoka upande huu, alikuwa mmoja wa wale wa kwanza kuwa katika Regional Assembly. Though kulikuwa na Parliament ya Nyumba mbili huko juu na halafu kwa every Province, kulikuwa na serikali ambayo ilikuwa na wajumbe na ilikuwa inaitwa Regional Assembly. Mmoja wenu hapa alitoka hapa kuwakilisha upande huu wote, upande huu ulikuwa unaitwa wakati huo Nyambene North hapa tu. Yaani upande huu Ntonyiri and Igembe ilikuwa Nyambene North hapa tu. Yaani upande huu and Ntonyiri and Igembe ilikuwa Nyambene North, that time. Mlikuwa na member wa Regional Assembly not National Assembly only, National Assembly kulikuwa na Mjumbe, mnajua? ----- alikuwa wapi? Ni National Assembly? (*in vernacular*) Regional Assembly at that time. Lakini hayo maneno yalibadilika sindio? Hiyo Constitution ilikuwa amended hiyo ikitoka.

Nikichukuwa point ingine, a person does not have to be a member of a party in order to stand for elections. Katika Constitution ya sasa, hii ambayo tunatumia leo, though hakuna Constitution ingine imekuja ni hii hii tu tunaendelea kutengeneza mpya tubadilishe hii, lakini kwa hii ni lazima uwe unaletwa na party ili uende Parliament, ama si namna hiyo? Lakini mapendekezo yale utaona huku si lazima uwe unapendekezwa na party peke yake, you can also be an independent candidate. Si unaona hiyo ni tofauti? Na hata hiyo mkikumbuka wale wazee kama Julius, mnakumbuka zamani kulikuwa na independent candidate. Si namna hiyo. Elections za 1963.

Interjection: inaudible

Com. Domiziano Ratanya: Unaona mzee anakumbuka, ----- alikuwa independent na alikuwa symbol yake ilikuwa Simba, nakumbuka. So that was there in the past, lakini si baadaye iligeuzwa? Ilikuwa amended, sasa hiyo ni tofauti moja.

Tukiangalia lingine unaona kwamba, MPs will no longer have power to fix their own salaries. Katika hii draft yetu (laughs) hiyo maneno tumepinga, unaona? Hawatakuwa na nafasi ya kuweka mishahara yao na tukiangalia kuzungumza utaona kuna Commission ambayo tunaita, Salaries and Remuneration Commission of Kenya. Commission itafanywa kama hiyo. Hii itaangalia mishahara yote.

Si group hapa kuenda kufanya mambo yake ingine pale, ingine pale. Ukiona sasa watoto wetu wako nje kwa sababu wale wanawafundisha wanakatazwa pengine pesa, hiyo Commission itakuwa inaangalia kila mtu. Kama ni walimu, kama ni Army kama ni nini, wote na MPs na Ministers. Hiyo Commission itakuwa ikiangalia mishahara yote kutoka hata ya President, itakuwa Commission ambayo itakuwa na nguvu ya kufanya hiyo kazi. Siku ya leo kuna hiyo Commission? Hapana. MPs wanaenda wanaketi kwa sababu wana ile nguvu ya kufanya sheria, wanasema, si lazima tufanye sheria yetu? Na hiyo yetu ni ya kutupatia nini? Kamshahara. Sasa hiyo mambo yatakwisha.

Interjection: Inaudible.

Com. Domiziano Ratanya: Sawa sawa namna hiyo. Sasa hiyo ni tofauti, nilikuwa tu nasoma hapa kuwaambia, how is the new Constitution different from the old. So I am picking just a few examples.

If I get another example here which is also becoming a new thing here is that there will be a new Supreme Court at the end of Judicial systems with all the new Judges.

Interjection: Inaudible.

Com. Domiziano Ratanya: Okey umeenda mbali kidogo kwa sababu nitakuja kwa Draft yenyewe, nitazungumza hiyo. Hiyo nime mention, we shall mention about Commissions kwa sababu kuna nyingi. Kwa hivyo tukimpatia hiyo example ya hapa tumesema, another difference is there will be a Supreme Court. Leo hatuna Supreme Court, lakini kwa kutoka kwa hii Draft Constitution mpya ikija kutakuwa na Supreme Court of Kenya. Tuko sasa mpaka Court of Appeal, lakini juu yake kutakuwa na Supreme Court na mtaangalia maelezo yake yako hapa. Na kama kunaye angetaka tukiingia hapo kuuliza, unaweza kuuliza.

Kwa hivyo hata hiyo ni tofauti. There is also something else, kitu ambacho kinaonekana kitakuwa kitu mpya, President mwenyewe atakuwa impeached. There is that impeachment of the President, yaani kukaguliwa na kuangaliwa kama amenfanya makosa, atengenezewe procedure mpaka aondoke. Lakini siku ya leo kuna hiyo mambo?

Audience: Hapana.

Com. Domiziano Ratanya: Hakuna. Na hiyo impeachment itaendelea kuna procedure yake pengine Bunge, na iende kwa Wazee wa National Council ndiyo watakuwa wanahusika sana katika Upper House. Hata hiyo pointi iko hapa. Na hata MPs,

recalling MPs. Mkiona huyo MP hamtakaa naye miaka mitano, amefanya mambo ambayo hamtaki, so there is that power to recall that MP, aje kwa nini? Arudi nyumbani, na akirudi nyumbani mfanye nini, mchague mwingine. Kwa hivyo kuna hiyo procedure, lakini siku ya leo kuanyo?

Audience: Hapana.

Com. Domiziano Ratanya: Kwa hivyo unaona hata hiyo ni difference.

Tukiangalia hata kwa hata ingine utaona kuna Administration Police. Hata hiyo kutakuwa na tofauti. Administration Polisi itakuwa katika kikosi cha polisi. Hakutakuwa hiyo, itakuwa yote polisi. Tulipokuwa tunachukuwa views kutoka kwa watu, wengi walisema, kwa nini tunaendelea kuwa na Administration Polisi hapa, hata ingine inaitwa Regular, si wote polisi? Kwa hivyo tuliposikia maoni yote na hata pengine nikisoma hapa kwenu hapa kuangalia hapa nitaona watu wa Ntonyiri walisema hivyo wengine. Hayo ni maoni ya watu kila pahali, na kwa hivyo tukaamua Administration Police iingie kwa polisi yenyewe, pengine ile sheria yao Cap 85 Laws of Kenya iwe repealed ama itupwe kabisa na tutumie Cap 84 which is Police Act wote waingie kwa police. Hakuna mtu atapoteza kazi yake. Yule ataondoka ni kawaida ya kuondoka yaani umri ama umefikisha retirement, ama umefanya makosa discipline lakini kutakuwa na kitu cha Inter Transitional Provision. Hiyo tutaangalia baadaye, nitawaonyesha kule iko wakati wa mabadiliko. Kama tukibadilisha kutoka kwa Police Administration iondoke kutakuwa namna gani? Wataenda kwa police na wakuwe accommodated namna hiyo. Kuna pointi ingine inahusika kama hiyo.

Provincial Administration: Provincial Administration will be abolished. Provincial Administration si utawala wa kule Embu ama Nyeri, ni utawala hii tunaita Provincial Administration. That system inanza kutoka kwa subchief. Hiyo ni system yote namna hiyo. Subchief ama Assistant Chief, the correct official title, Chief, D.O, D.C. na P.C halafu P.S ambaye anaitwa kusimamia Provincial Administration. Hiyo laini yote ndiye nini? Provincial Administration. That will be abolished na hiyo ikiondoka, mtaona vile itarudishwa ile kazi walikuwa wanafanya haitapotea. Unajua kazi ndiyo ya muhimu. Ile walikuwa wanafanya nzuri ambayo inatajikana wananchi itarudi. Lakini kama kuna mambo mabaya wanafanya kama corruption, kama mambo mengine. Hayo hayatarudi. Wanainchi watapata utawala umepangwa kwa njia nzuri. Sasa system hiyo inaonekana itapotea kabisa na hayo yalikuwa ni maoni ya wananchi kila pahali.

Is there any point you would like us to highlight, I will not go through all of them. Now katika serikali yenyewe mpango kutoka Nairobi mpaka kwenda kwa wananchi, wananchi walikuwa wanataka sana kuwe na devolution of power yaani utawala uende kwa wananchi, uwe shared si ukae na mtu mmoja. Na nikiangalia hapa kuna pointi kama hiyo na baadaye tutasoma kwa draft yenyewe. There will be a system of the devolved government, which is entrenched in the Constitution and based on the districts, though this will also form a Provincial Council, there must also be a village and a Location Council. Hiyo tutaangalia contract yenyewe pahali na hata hapa kuna diagram ambayo nitawaonyesha. Mtaona serikali vile inagawana power kutoka juu, kutoka Nairobi inafika kwa district ndiyo itakuwa kile kiwango kikubwa sana halafu locations, halafu village. Maana yake ni kuhusisha mwananchi kutoka district level. Watu walikuwa wanalalamika eti serikali kila kitu inafanyiwa Nairobi. Ukitaka

kabarabara kadogo kajengwe, mambo yanaandikwa hapa yanaenda Nairobi. Sasa mambo mengi yatakuwa yanafanywa kutokana na wananchi wenyewe. Na hapa nina diagram ambayo ningetaka kuwaonyesha hata ingawa hamna hii kitabu I shall show you this one which I have, on page 45 mkisoma kwa Documentation Centre ambayo mtapata hiki kitabu huko, mtaona kuna diagram hapa imepigwa ya kuonyesha hiyo devolution of power. Yaani ku-share power kutoka Nairobi, kutoka Central Government. Hapa tuna-mean wale ambao wanatawala Kenya are the people, yaani mwananchi wa Kenya ndiye mkubwa zaidi. Ndiyo mnaona tunanza huko juu, the people. Kwa sababu hata hii Katiba imetengenezwa na nani? Ni wananchi, it's the people's Katiba. Ya kwanza ilitengenezwa huko London na viongozi, lakini imekuja hata nyinyi mnaketi hapa na mnaizungumzia kuitengeneza. This is why we say it is people driven na juu ikiwa people, hawa watu ndiyo wanachagua mtu wa kuwatawala kwa niaba ya watu, anaitwa President akiwa mtu wa kwanza. Below President, kuna Vice President, hapo chini kuna Prime Minister tena kutakuwa na Deputy Prime Ministers wawili na wataonyeshwa kazi zao, then ministers. Sisi tulionelea kulingana na maoni ya wananchi kuwe na only 15 Ministers na 15 Assistant Ministers. Na hata hawa Assistant Ministers, hatuwaiti Assistant kwa Draft yetu. Tunawaita Deputy Minister. Kama Prime Minister haitwi Assistant, anaitwa Deputy Prime Minister.

Na kutoka hapo, kuna Councils ambazo zitakuwa huko juu kwa Central Government, tutakuwa na Council moja inaitwa National Assembly, that is the Parliament. The Parliament will have two Chambers, moja inaitwa National Assembly na ingine inaitwa National Council. National Assembly itakuwa na 210 MPs kama vile walivyo sasa. From Ntonyiri, from Igembe, from everywhere, one, one, one kama vile walivyo 210, hao ndiyo watachaguliwa namna hiyo tukiwachaguwa tena, tutachaguwa 210 in Kenya, na kutakuwa na wengine 90 kuongezea hawa ile kuwakilisha sehemu mbali mbali ambazo haziakilishwi ama pengine zina baguliwa, kama akina mama, kama disabled, kama tribes ambazo ni wachache sana, maybe professionals, na hapa real number ni 90. kwa hivyo National Assembly itakuwa wangapi? 300 members. National Council, itakuwa na mmoja kutoka kwa every district. Na tunaona kwa ma-record districts ni 69, kwa hivyo watakuwa 69. Nairobi itachukuliwa kama district, hiyo ni moja. Kwa hivyo watakuwa wangapi? 70. Halafu kutakuwa na wengine 30 to represent women's interest, na hao watachaguliwa kutoka kwa province. Kila province one, provinces 7, hao ni 28, kila moja one. Na kutakuwa na wawili kutoka Nairobi alone, kwa hivyo ni 30. Sasa hii kazi itakuwa na 100 members. National Council ambayo is a sought of the Upper House.

Now still the Government will devolve down to the district. Kutoka Nairobi sasa ile itakuwa na nguvu zaidi, ni district ambayo itakuwa na district council. Sasa tunaiitaje? Ya district inaitwaaje sasa? County Council. Lakini unajua within the district leo, tuna hata Municipal Council si ndio? Kuna hata County Council, na mnaona vile vinaingiliana. Katika County Council inazunguka district yote, lakini ndani yake kuna town ambayo inaitwa Municipality ina mkubwa anaitwa Mayor. Sasa hiyo mambo itaisha. Kutakuwa na Council moja ya nini? Ya district. Hata district itakuwa na Council moja. Na wajumbe watatoka kutoka kwa wards zile ziko sasa ama locations, na wakati huo pengine kutafanywa regulations ya kuonyesha boundaries, kama kunayo intaongezwa ama ipunguzwe. The Parliament will make those regulations.

Kutoka district tutaeda kwa Locations. Locations nazo zitakuwa na Councils, itakuwa na elected people kutokana na zile boundaries ambazo zitawekwa na Parliament, kuonyesha what do we mean by a Location. Pengine Location inaweza kuwa ni present division we don't know, lakini itafanywa.

Na halafu tutaenda kwa village. Na hapo village, watu wengine wanafikiria village ni watu wachache pengine nyumba mbili, tatu, nne. Hiyo village itakuwa defined, kuna watu wanafikiria village inaweza kuwa na watu kama 3000 to make a village or 5000 to make what we call a village. Ile village mna watu wawili watatu, kama ni Julius na family yake na mwingine, hapana. Hiyo tu ni jina ya kuonyesha tunaenda kwa wananchi. Hata hiyo pengine inaweza -----

Na Province kutakuwa na Council. Lakini Province kutakuwa na representatives wa district ndiyo wataenda huko wata-form a sought of a Council katika Province. Kazi yake itakuwa tu kuunganisha ma-districts. Haitakuwa na nguvu nyingi kama hii ambayo ni ya district. Kwa sababu district itafanya hata sheria zake. Sheria nyingi ambazo zinahusika na watu wa hapo zitatengenezwa kwa district level. Kwa mfano nikifikiria sheria kama moja ama mambo fulani kama mambo ya miraa, hapa hapa tulisikia eti miraa ni lazima iingie kwa njia nzuri. Ni zao nzuri sana kwa sababu inatusaidia kwa economy tunapata pesa na maendeleo yanatokana na miraa. Hata Commission imeweka miraa kuwa na maana sana. Watu wengine tukienda huko upande wa Coast, tunasema mambo ya fish, samaki, kuna wengine wanasema mambo ya karafuu, pale iko. Si unajua kila watu wana vitu vyao. Tukienda huko Modogashe, wanasema lazima hii mifugo yetu tujue tutauza wapi. Wanataka Factory, ili tuwe na pahali pa nyama na wawe wanauza. Kwa hivyo mambo kama haya ambayo ni tofauti tofauti, hayo tumependekeza yawe yanafanywa kwa district level. Kwa sababu district ndiyo itafanya sheria nzuri ambayo watu watatosheka. Na hata hiyo itakuwa kwa Katiba na hata sheria ya nchi yote, yaani kwa National Assembly and so on.

Tuseme sasa mambo ya miraa yenyewe, District Council ikikutana, kwa sababu hii District yetu Meru North, tunahusika sana mambo ya miraa, miraa ni kitu yetu na tunapenda, watu wengine wanasema ni kama pombe, lakini sisi tunajua miraa ni kitu cha maana. Kwa hivyo District Council itakutana ifanye sheria. Vile wanataka miraa kama ni kuuzwa, kama kutengenezwa kwa njia fulani, kama ni kupeleka pahali, watafanya sheria kwa District level na hiyo sheria itaenda mpaka ikubaliwe kwa serikali, na watu wa hapa wafaidike kwa hiyo. Hatuwezi kuweka sheria pengine na kutawala mambo ya miraa kwa Mujaluo ambaye hana miraa. Kweli ataheshimu hiyo? Kwa hivyo kule Siaya, huwezi kuambia Council ya Siaya iketi ifanye sheria ya miraa. Itawezekana, huko watafanya sheria ya samaki kwa sababu wako karibu na lake. Mambo yao huko ni samaki, samaki. Tukienda mambo ya karafuu, na ingine, tukienda huko Mombasa, pengine watafanya sheria hiyo kali sana, kusaidia watu wao na economy ya area hiyo. Kwa hivyo usiseme miraa ya kwamba haikuingizwa katika Draft, imeingizwa sana sana na ndiyo itatengenezwa na hiyo Council ya District. Itafanya sheria na hiyo sheria itaheshimiwa, na watu watatosheka na watafaidika.

Nikitoka kwa hii sasa kwa sababu hii niliwaambia ni report ambayo ina-cover mambo generally, na nimesema machache yale tumechukua kwa Constitution, hii report ina andamana sana na yale mambo mlitwambia. Kutokana na hii report ambayo tuli-launch tarehe 18 September, na mambo yenu ambayo yametoka kwa Constituency, tulipo keti, tuliangalia vizuri mpaka

tukafanya mapendekezo ya Katiba. Sasa hii naguza hapa ni mapendekezo ya nini? Ya Katiba yenyewe. Haya yakipita kama vile yalivyo vitabu vitaandikwa vikiwa namna hiyo hiyo tu, na iitwe Katiba ya Kenya, nikimaliza all those things. Lakini hii niliwaambia hii yenyewe hatuwezi kusema hii ni Katiba siku ya leo. Haijakuwa Katiba, ni mapendekezo ya kutengeneza Katiba yetu mpya ya Kenya. Na siku ya leo nimewaletea ili msome muanze kusoma, kuulizana maswali, kufanya corrections pake unaona si nzuri. Pale unaona ni mzuri unakubaliana nao, pale unaona si nzuri unafanya amendment na baadaye utaandika report yako.

After 30 days kila mtu atakuwa amesoma ama group. Mtasoma in groups, kama mna makundi ya akina mama, makundi ya wazee, makundi ya walimu, makundi ya vijana disabled what, mtaketi mtasoma hii Katiba na hata ukiwa individual ama wewe ukiwa peke yako tu na family yako, mtaketi mtasoma na halafu mtafanya comment. Pengine mnaweza kusema kitu ambacho tumesema hapa kingine si kizuri, na uandike argument yako, uandike sababu yako ya kusema si kizuri. Ama useme ni kizuri ama useme mambo mengine yameachwa hayakuingia kama vile unasikia watu wengi wengine wanasema, mambo ya wafanyi kazi, labour haikuwepo sana, hiyo ni malalamiko itaangaliwa. Na mkiandika hayo malalamiko yataenda kwa Commission, lakini lazima yawe in writing, yakienda kwa Commission, Commission inatengeneza mkutano wa National Constitutional Conference ambayo itakuwa tarehe 28, na utakuwa na 30 days ya kwenda through hii, hii ukiangalia na ukifanya uchunguzi wako wote na ukifanya corrections ama kuongeza.

National Conference, wananchi wamechagua Wajumbe watatu kutoka kwa kila district na district zote kama ni seven, kama ni watatu watatu, unaweza kufanya hiyo hesabu haraka useme ni wangapi? 210 straight away, ile hesabu yetu ya zamani carry ----- computer ya kichwa, 210. 70 x 3 is 210. Hawa 210 wametoka kwa district watatu watatu. District ina watatu na mmoja ni lazima awe ni mwanamke. Na hapa hapa tuko kuna mjumbe mmoja ambaye alichaguliwa kwa Meru North. Mama ambaye ni mmoja wa wale watatu. Pengine mngetaka kumjua huyu madam Beatrice Mbario. Huyu pengine mnamjua sana, okey. Mnaona sasa hamjui delegate anatoka nyumbani? Huyo ni mmoja, kuna mwingine hapa hapa anaitwa Counillor, I don't know kama huyo yuko around, alikuwa hapa hapa.

Audience: Inaudible.

Com. Domiziano Ratanya: Okey, sasa huyo ni mtu wa kwenda Nairobi huyo. Mwingine ako hapa. Mwingine naye wa kufanya watatu kwa district hii ametoka Mikinduri huko karibu na ----- karibu na mpaka wa Tharaka. Unaona district imekuwa covered? Sasa hawa watatu wataenda Nairobi na ndiyo tunawaita delegates wetu, ambao wataakilisha Meru North District. Na kutakuwa na wengine kutoka makanisa na majina mengine ya hawa watu hapa lakini mtawajua baadaye. Kuna wakutoka makanisa, kuna wengine wa kutoka kwa groups za akina mama, NGOs, na tena wengine ambao watakuwa huko ni Wajumbe wenu wale wako sasa. Ni wangapi? 210 kwa sababu kuna 210 Constituencies. Tena wale Wajumbe wengine watakuwa huko ni Commissioners, sisi tutakuwa huko 29 lakini hatutakuwa na kura, hiyo ndiyo itakuwa tofauti. Kwa sababu tumefanya hii kazi yote ambayo mmetupatia kama wananchi katika Kenya, kufanya draft, na sasa kuwa na kura kwa sababu

hatuwezi kupigia hii document yetu kura. Wale watakuwa na kura ni akina Beatrice, Councillor huyu ambaye ako hapa na wengine, na hata MPs watapiga kura. Lakini sisi kazi yetu ni kufanya mipango ya hiyo conference iendelee na iwe inafanyika sawa sawa. Yaani kufanya pale wataketi, kufanya maybe documents, mipango hiyo yote, hiyo ndiyo ni kazi ya Commission na tutakuwa huko lakini hatutakuwa na uwezo wa kupiga kura. Sheria imetukataza hiyo, sheria ambayo inatutawala ambayo tunafanya kazi nayo hii Constitution of Kenya Review Act Cap 3A ndiyo inatueleza ile kazi Commissioner wanafanya.

Sasa group yote ambayo itakuwa National Conference watakuwa kama 600 hivi, around there. Hawa wakikutana Nairobi wataangalia hii draft ambayo inafanywa na Commissioners, na tena waangalie maoni yenu kutoka kwa hii draft, yale ambayo mtaandika mpeleke huko. Hayo ndiyo watazungumza na watakaa kama 30 days hivi, itakuwa ni kazi nyingi kwa sababu watakuwa wanaenda kutoka paragraph, kutoka page, yote wataangalia mpaka baada ya 30 days, wawe wametoka na repoti yao. Wakikubaliana eti hii sasa imekuwa sawa na hakuna malalamiko na hakuna ubishi, hii tunaita consensus, wakubaliane kabisa ama kama ni kura waseme na kura wamekubaliana. Hiyo sasa itakuwa ni report ambayo itatengenezwa na draftman wetu, halafu itapelekwa Parliament, ikiwa sasa Draft Bill ambayo itaenda kufanya sheria na Parliament, na Parliament ikimaliza hapo, itakuwa sheria, yaani itakuwa sasa Katiba ya Kenya. Itakuwa Constitution ya Kenya ki-sheria.

Hebu tuseme kwa mfano hawa members ambao watakutana 28th na wanaendelea mwezi moja, wasipokubaliana na hatuombi wakatae kukubaliana, tunataka watengeneze hii mambo iwe wamekubaliana ifanywe haraka. Lakini wakikataa, sheria inawaambia kwa hii kitabu ama amendment yake ambayo nina hii, kwa sababu hata hii imekua amended tena, inasema, wanaweza kupeleka haya mambo kwa referendum yaani ile tunaita kura ya nini? Ya raia. Kama kuna kitu hawataki kusikizana, sheria inawakubalisha wapeleke kwa wananchi wakapige kura. Ndio utaona yatakuja kwenu huku tena kwa polling stations, mpigie Katiba Kenya. Hiyo hatujui kama itafika hapo kwa sababu mambo haya yote yamefanywa vizuri na Commissioners. Hawa delegates wataketi kwa hii mambo vizuri na tunafikiria na tunaomba mambo yaishie kwa delegates. Si namna hiyo? Lakini kisheria nimewaambia kwamba mnaweza kuendelea kwa sababu wengine hapa wataniuliza, delegates wakikataa kukubaliana itakuwa aje? Sasa Ndiyo nawaambia, wasipokubaliana wana hii njia ingine ya kwenda ambayo ni referendum. Lakini kwa kawaida hiyo haisikiki. Nafikiria hawa members watakubaliana.

Sasa kuna kitu kingine kabla ya kuangalia hata ndani kwa sababu tutaangalia hii ndani, tutachukua mifano ndani. Kazi ya Commission yenyewe niliwaambia nataka kuhimiza hapo, tulimaliza kazi ya ku-draft Constitution na kwa kufanya hii, mambo yale mengine yamebaki, kweli utaweza kulaumu Commission? Yale yamebaki tu ni mpango kwenda tu kwa Constitutional Conference, mpango kwenda kwa Parliament. Mpango pengine wa elections. Hayo yote si kazi sasa ya Commission. Lakini kwa vile tumechukua maoni hata tukisoma hayo maoni yote kwa 210 Constituencies, watu wanasema Katiba ikiwa tayari before December, si waifanye kwa new Katiba? Wengi, I think Kenya yote hata ukisoma huko hata Commission, tunakubaliana nayo, ifanywe na new constitution. Lakini hatuwezi kuweka sisi kwa sababu hiyo si kazi yetu, lakini tunganee tunakubaliana na maoni yale tulipewa na nini? Na wananchi. Lakini kuifanya eti ifanywe na new constitution ama old constitution, commission haiwezi kufanya hiyo kazi, hiyo ni ya mtu mwingine. Si ndiyo? Hiyo ni ya wengine. Mnasikia sasa hii

inaenda kwa National Conference na Commission haina kura, tutahimiza hayo mambo na hatuna kura, hatuwezi. Haya mambo yataenda kwa Paliament Hatuendi Parliament. Sasa Parliament na delegates wale watakuwa National Conference na Serikali yenyewe ambayo iko sasa, hiyo sasa itakua mambo yao kuona ya kwamba kama tutaenda na Katiba hii hii mpya ama Katiba ya sasa ni wao wataamua. Msilaumu Commission hapo, Commission haina mamlaka hayo. Hata hao watu wanasema mambo ya kuvunja Bunge nini, hiyo in prerogative ya President. Hiyo ni kazi ya President, hiyo si kazi ya sisi Commission. Kazi yetu tumefikia wapi? Hapa kufanya draft. Na ile sasa kazi tunaendelea nayo kutoka sasa baada ya hii draft ni kupanga mipango mpaka ifike mwisho yaani ni kama kazi sasa ya official tu ya ukarani tu, kupanga vile hao delegates wataketi, ni nyumba gani, makaratasi gani, officers wale wataandika na ma-computer, hiyo yote ndiyo tuna-coordinate, na hao wakimaliza, tuone kwamba draft inaandikwa vizuri ili iende Parliament, hata hiyo ni kazi yetu, lakini kwa decision, decision yetu imeishia kwa hii. Uamuzi wetu umeishia kwa hii, na ikiwezekana ikisemekana itakuwa referendum hata hiyo itaonekana njia ya kupanga hata hiyo, lakini tunafikiria itaishia kwa National Conference.

Sasa tukifika kwa hayo msiniambie sana niwaambie kama itakua hivi na hivi, pengine mmesikia yale nimesema uwezo wetu umeishia hapa na wengine ndiyo watatusaidia wasikie malalamiko ya wananchi katika Kenya yote na wafanye vile wananchi pengine wanasema.

Hebu twende kwa hii draft yetu, kwa sababu mtaendelea kusoma, hatutasoma yote, naamini kwa launching ningetaka kufanya introduction tu, tuone vile tutaisoma, ili usifikirie hii ni gazeti ya kawaida. Yenyewe ni Nation, lakini unaona imewekwa mambo mbali. Kwa hivyo usiweke mambo mbali huko kama Nation, ikiwezekana hii weka ya history mpaka hata babu zenu wawe wakiona pale Katiba ilianza. Enda uweke kabisa pale unaweka kitu chako cha muhimu, labda kwa file baada ya kusoma. Na tuone vile tunaendelea kuisoma. Fungua page 1, lets say page 2. Page 1 hapa juu mnaona it was issued on 27th day of September 2002. Page 2 hapo juu chini ya Constitutional Republic of Kenya, kuna table of contents, mnaona hapo. Arrangements of articles. Hii section tunaita articles kwa hiki kitabu, kwa Constitution ambayo tunayo sasa tunaita sections. Lakini tumependelea kwa draft yetu kuiita articles. So you see the arrangements of articles. Arrangements of articles kuna chapter 1, ambayo inaanza na article 1 ambayo inasema sovereignty of the people. You see then the supremacy of the Constitution, enforcement of the Constitution, defense of the Constitution, the laws of Kenya. Hiyo sasa ni chapter 1 ambayo iko na hayo mambo na yako ndani aambayo ni tayaangalia pale yako, tena utaenda chapter 2, utaenda zingine chapter 3 mpaka mwisho, hiyo ni arrangements ya chapters.

On page 3 utaenda chapter 20, ya mwisho ni Transitional and Consequencial Provision. Na utaona hapa kuna action of Parliament Transitional and Consequencial Provision na kutakuwa na schedules, yaani tables and so on. Now kwa hii sasa kabla hatujaenda ndani kabisa (inaudible). Now kitu kimoja ningetaka mjue, kwa arrangement ya articles zetu kutoka chapter 1, ending ya chapter kama hapa chapter 1 ending ni sovereignty of the people and the supremacy of the Constitution. Hiyo ndiyo ending. Ending ya draft yetu inawekwa juu ya maelezo, lakini kwa hii Katiba ya leo, hii the current Constitution wale ambao wamesoma imewekwa kwa paragraph. Ending inawekwa kwa paragraph. Mnaona hii inawekwa hapa? Inawekwa

